

OFISI YA RAISI-TAMISEMI

HALMASHAURI YA WILAYA YA KYELA

SHULE YA SEKONDARI KATUMBASONGWE,

S.L.P 138,

KYELA.

.../.../2021

Kumb. Na. KDC/S3126/VOL1/018

JINA LA MWANAFUNZI

S.L.P.....

KYELA.

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KATUMBASONGWE MWAKA 2021

1.0. UTANGULIZI.

Ninayo furaha kukuarifu umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2020. Shule ya sekondari KATUMBASONGWE ipo umbali wa Km 10 magharibi mwa mji wa kyela. Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe 04/01/2021 unatakiwa kuripoti shuleni tarehe 04/01/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 11/01/2021. Unatakiwa kufika bila kukosa.

2.0. Mambo muhimu ya kuzingatia

2.1. Sare ya shule

a) Wavulana.

Suruali nadhifu mbili, moja rangi ya damu yam mzee na nyingine rangi ya bluu bahari, mashati mawili ya mikono mifupi.

b) Wasichana.

Sketi nadhifu mbili (ndefu) moja rangi ya damu ya mzeena nyingine bluu bahari, mashati mawili ya mikono mifupi.

Hijabu (kwa waislamu) kitambaa lazima kifanane na rangi ya shati.

c) Sweta damu ya mzee

d) Viatu vya ngozi vyeusi vya vifungwavyo kwa kamba jozi mbili. Ni marufuku kuvaa viatu vya plastiki (yebo yebo)

e) Soksi nyeupe ndefu (wasichana) na nyeusi (wavulana)

f) Sare za michezo ni track suit rangi ya blue bahari na viatu vya michezo (zitakaguliwa shuleni)

2.2. Daftari za kutosha (counter book quire 3) kalamu na mkebe wa hisabati.

2.3. Chakula cha wanafunzi (wa kutwa) nauli ya kwenda shuleni na kurudi nyumbani pamoja na matibabu

2.4. Mzazi au mlezi anapaswa kuhudhuria vikao vya wazazi vitakavyoitishwa shuleni.

3.0. Sheria na kanuni muhimu za shule hii

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu na 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa sheria na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya elimu sayansi na teknolojia na mafunzo ya ufundi yenye dhamana ya elimu nchini na ofisi ya raisi TAMISEMI. Utumishi na utawala bora yenye majukumu ya usimamizi na uendeshaji elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

- a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
- c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)
- d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
- e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani.
- f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
- g) Kuvaa sare ya shule wakati wote.
- h) Kutunza mali za shule.
- i) Kutokuwa na simu ya mkononi.

3.1. Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule.

- a) Wizi
- b) Uashereti
- c) Ushoga
- d) Ubakaji
- e) Matumizi ya dawa ya kulevya
- f) Kupigana au kupiga
- g) Kuharibu kwa makusudi mali ya shule
- h) Kudharau bendera ya taifa
- i) Kuwa mjamzito au kusababisha ujauzito
- j) Kuoja au kuolewa
- k) Kutoa mimba
- l) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
- m) Kukataa adhabu kwa makusudi
- n) Kumiliki simu ya mkononi.

4.0. Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi .

- a) Medical examination form ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakapo ripoti shuleni.

- b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
- c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelezo mengine yatakayotolewa na shule.

5.0.TAFADHALI SOMA KWA MAKINI MAELEZO/MAAGIZO HAYA NA KUYATEKELEZA KIKAMILIFU.

Karibu sana katika shule hii

.....

NCHIMBI A.B.

MKUU WA SHULE-0757208633